KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 22, Issue 4
4th Rajab 1433
25th MAY, 2012

Tabia Njema, Kutenda Wema na kuwa na Mafungamano Mazuri.

NA: SHEIKH MUHAMMAD NAASIR UD-DEEN AL-ALBAANI (رحمه الله)

Amepokea Abud-Dardaa' kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa amesema: "*Jambo lenye uzito mkubwa zaidi kwenye mizani ni tabia njema."* [No.876]
Imepokewa na Abu Hurairah kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba amesema: *"Mtu akisema 'A'oodhubillaah'* anapokasirika, basi hasira zake huondoka." [No.1376].
Imepokewa na Abdullaah Ibn 'Amr Bin al-'Aas yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Kuweni na huruma, na utawahurumia. Sameheni na Allaah atawasamehe. Ole wao wale wenye kusikiza kama bomba (hawatekelezi wala hawajali wanayoambiwa). Ole wao wale wenye madhambi ya waziwazi, na wakadhihirisha madhambi yao ingawaje wakawa wanajua yakuwa waliyoyafanya ni makosa."* [No. 482].
Amepokea 'Ubaada kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Nidhaminini mimi kwa mambo sita katika nafsi zenu nami nitawadhaminia nyinyi Pepo: Kuweni wakweli munapozungumza na mutekeleze ahadi zenu, tekelezeni amana, hifadhini tupu zenu na muangushe macho yenu na muiepushe mikono yenu na kugusa!* [No. 1470].
Imepokewa na 'Abdullaah Ibn 'Amr: yakwamba Mu'aadh Ibn Jabal aliazimia kusafiri, kwahiyo akamuuliza Mtume (صلى الله عليه وسلم) amnasihi. Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Muabudu Allaah na usimshirikishe na kitu chochote."*
Akasema Mu'aadh: "Yaa Rasoolullaah, niambie zaidi.". Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *"Unapofanya jambo la makosa liandamize na jambo jema."*
Akasema Mu'aadh: "Yaa Rasoolullaah, niambie zaidi". Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *"Kuwa na msimamo mzuri na ufanye tabia yako kuwa nzuri.* [No. 1228]
Amepokea Abu Sa'eed al-Khudhree' kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Waumini wakamilifu katika Imani zao ni wale wenye tabia njema, ambao ni wanyenyekevu, wenye kuzifungamanisha nyoyo zao na nyoyo zao zikafungamanishwa. Hapana wema kwa yule asiyezifungamanisha nyoyo wala moyo wake usiofungamanishwa."* [No. 751].
Imepokewa na 'Abdullaah Ibn 'Amr aliyesema: "Siku moja Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuja nyumbani kwetu mimi nilipokuwa badoi ni mdogo, nikatoka nje ili nikacheze. Akasema Mamangu: 'Ewe Abdullaah! Hebu njoo hapa nitakupa kitu.' Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *"Umekusudia kumpa kitu gani?* Akajibu*: Nilikusudia kumpa tende."* Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Lau kama hungelimpa kitu chochote, basi ungeliandikiwa urongo dhidi yako."* [No. 748].
Amepokea Aayaad Bin Hamaar, kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba aliwatolea khutbah akawaambia: *"Kwa hakika Allaah ameniteremshia mimi yakwamba munahitajika kuwa ni watu wanyenyekevu kiasi cha kwamba pasipatikane kuwa yoyote miongoni mwenu na kiburi, akainuliwa juu ya mtu mwengine. Wala mtu yoyote asimdhulumun mwenziwe."* [No. 570]
Katika mapokezi ya Rabeeyah al-Aslamee aliyesema: Nilikuwa nikimuhudumikia Mtume (صلى الله عليه

'ILMU YENYE MANUFAA

"THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA" [QSSEA] WANAWAALIKA MIHADHARA YA KI-'ILIMU KATIKA MASJID MAZRUI KUANZIA TAREHE 31st MAY – 3rd JUNE, 2012 [SIKU NNE]

WAKATI WA MIHADHARA:

KUANZIA BA'DAL ASR MPAKA ISHAA'. 4:15pm - 'ISHAA'

MADDA ZITAKAZO ZUNGUMZWA:

- *ATHARI ZA MADAWA YA KULEVYA.
- *MAMBO YENYE KUHARIBU IMANI YA MTU.
- *ADABU ZA MA-SALAF ZILIVYOKUWA.
- *HUKMU ZA SIHRI (UCHAWI) KATIKA UISLAMU.
- *ATHARI ZA TALAKA KATIKA MUJTAMA'
- *MALEZI BORA KATIKA UISLAMU.

YALIYOMO

TANGAZO LA DARSA	1
TABIA NJEMA	1 - 3
SWALA YA NYUMBANI	3 - 4
DA'WAH KWA -	-
- WASOSWALI	4

(Endelea Kutoka Uk. 1)

وسلم) akanipa kipande cha ardhi, na pia akampa Abu Bakr kipande cha ardhi. Ilipofikia katika kuigawa ardhi hiyo, tukagombana juu ya shawi la tende katika mtende mmoja. Abu Bakr akasema: "Shawi hili liko kwenye sehemu yangu ya ardhi!" Na mimi nikasema: "Liko kwenye sehemu yangu ya ardhi!" Pakawa na mushkili baina yangu na Abu Bakr, kisha Abu Bakr akatokwa na maneno ambayo hayakunipendeza, lakini baadae akajuta kuyasema maneno hayo, basi akaniambia: "Ewe Rabeeyah! Na wewe niambie neno kama hilo nilokwambia wewe, ili lipate kulipa kisasi." Nikamwambia: "Mimi sitolisema neno hilo." Akasema Abu Bakr: "Utalisema au nitamuomba Mtume (صلى الله عليه وسلم) akuamrishe kulisema." Nikamjibu: "Sitolisema." Abu Bakr akaniwachia hiyo sehemu ya ardhi na akenda kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) - nami nikaanza kumfuata. Watu wa kabila langu nao wakaanza kutufuata, wakaniambia: "Rehma za Allaah zimshukie Abu Bakr, mbona anakwenda kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) - kukuhusu wewe?" Basi nikaanza kuwaeleza, "Nyinyi mwamjua huyu? Huyu ni Abu Bakr as-Siddeeq, yeye ni mmojawapo wa wawili waliokuwa kwenye pango, naye ni mmoja aliyezeeka kama Muislamu (Mmojawapo wa wazee wa Waislamu), jitahadharini asije akageuka nyuma na kuwaona nyinyi mukitaka kunisaidia mimi dhidi yake, akakasirika, kisha akamuona Mtume (صلى الله عليه وسلم), mara Mtume (صلى الله عليه وسلم) nae akakasirika kutokana na kukasirishwa (Abu Bakr), kisha Allaah (سبحانه وتعالى) nae akakasirika kutokana na kukasirika kwao na kisha Rabeeyah ataangamia." Wale jamaa zake wakamuuliza Rabeeyah: "Sasa watuamrisha sisi tufanyeje?" Nikawaambia: "Rudini zenu." Abu Bakr akaelekea mpaka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), nikawa mimi peke yangu namfuata huko mpaka akafika kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Abu Bakr akamueleza Mtume (صلى الله عليه وسلم) kisa chote kama kilivyokuwa. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akainua kichwa chake kuniangalia mimi kisha akasema: *"Ewe Rabeeyah, kuna nini baina yako na as-Siddeeq?"* Nikasema: "Ewe Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) - kumetokea kadhaa na kadhaa, kisha akaniambia mimi maneno niliyoyachukia, kisha akaniambia, na wewe niambie maneno kama hayo niliyokwambia ili uwe umenilipiza, lakini mimi nikakataa kufanya hivyo." Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasma: *"Ndio usimjibu kwa maneno mabaya, na badala yake sema: 'Namuomba Allaah akusamehe ewe Abu Bakr. Allaah akusamehe ewe Abu Bakr."* Hasan akasema: "Abu Bakr akageuka na huku alikuwa akilia." [No. 3258]

Imepokewa na Anas aliyesema: Yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwambia mtu fulani: "Ewe fulani wa fulani! Wewe umefanya kadhaa na kadhaa?" Akajibu yule mtu, "Laa! Mimi naapa kwa Jina la Allaah, ambaye hapana mola apasae kuabudiwa kwa hakki isipokuwa Yeye tu, mimi sikufanya!" Mtume (صلى الله عليه وسلم) alijua yakwamba kwa hakika amefanya hilo jambo, basi akamwambia: *"Kwa hakika Allaah ameshakusamehe urongo wako, kwa ajili ya kuiyakinisha kwako 'Laa ilaha illa-Llaah.'"*

Imepokewa na Abdullaah aliyesema yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "*Kwa hakika Allaah amewagawanyia adabu zenu (tabia njema) baina yenu kama alivyowagawanyia riziki zenu baina yenu.*

Allaah humpa Duniya [Ulimwengu] kwa ampendae na asiyempenda, lakini hampi Imani isipokuwa yule ampendae.

Mtu yoyote aliye bakhili katika kutumia mali yake, na muoga katika kupigana na adui, na dhaifu mno katika kusimama usiku kwa ajili ya swala, basi na aseme, 'Subhaanallaah, wal-Hamdulillaah, wa-Laa ilaaha illallaah , wallaahu Akbar.'" [No. 2714]

Amepokea Miqdam Bin Ma'adee Karb al-Kindee kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyesema: *"Kwa hakika Allaah anawaamrisha kutekeleza haki za mama zenu, kisha mutekeleze haki za jamaa zenu wa karibu na kisha wale wanaokuja baada yao."* [No. 1666].

Imepokewa na Anas kuwa amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa na Ngamia-Jike aitwae al-Udbaa', na hapakuwa na aliyeweza kumshinda katika mashindano. Siku moja akaja Mbedui na Ngamia wake, akamshinda al-Udbaa'. Jambo hilo likawa ni zito mno kwa Waislamu, wakashangaa kwa kushindwa kwa al-Udbaa'! Juu ya tukio hilo, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema*: "Kwa hakika, ni katika haki za Allaah , yakwamba hakinyanyui (hakiinui) kitu chochote katika ulimwengu huu, isipokuwa mwishoe hukishusha."* [No. 3525].

Imepokewa na 'Aaisha aliyesema yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Kwa hakika mtu hufikia daraja ya mwenye kuswali swala ya usiku na kufunga katika wakati wa mchana, kutokana na tabia yake njema."* [No. 795].

Amepokea Umaarah Bin Khuzaymah bin Thaabit yakwamba babake alisema: "Niliota kama kwamba nilikuwa nikisujudu juu ya bapa la uso wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Nikamjulisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusu ndoto hiyo, nae akaniambia: *"Kwa hakika roho hukutana na roho nyengine* [katika riwaya nyengine: keti chini, sujudu na ufanye uliyoyaona]". Mtume (صلى الله عليه وسلم) akakipetesha kichwa chake namna hii - [Akasema 'Affaan: kwa kukiinamisha kichwa chake nyuma] - kisha akaweka bapa lake la uso juu ya bapa la uso wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). [No. 3262].

Imepokewa na Abu Hurairah: Yakwamba mtu mmoja alisema: "Ewe Mjumbe wa Allaah! Kwa hakika mimi nina jamaa zangu wa karibu sana, na ninachunga sana uhusiano nao lakini wao hawanijali. Mimi ni mzuri kwao lakini wao ni wabaya kwangu. Mimi ni mkarimu kwao lakini wao ni wakali kwangu. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *"Lau kama ilivyo ni kama usemavyo basi ni kama kwamba wewe unawalisha majivu ya moto, wewe utaendelea kupata usaidizi kutoka kwa Allaah maadamu wewe unaendelea kuwa katika hali hiyo."* [No. 2597].

Amepokea Anas Bin Maalik yakuwa amesema: "Baadhi ya wageni kutoka Bahrein walikuja kumzuru Mtume (صلى الله عليه وسلم). Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaagizia maji kwa ajili ya Wudhoo' (kutawadha) na akatawadha. Wakaanza kuyakimbilia maji ya wudhoo' wa Mtume (صلى الله عليه وسلم), na wakanywa katika maji hayo kiasi walichoja'aliwa. Na yale maji yaliyomwagika kwenye ardhi walijipangusia nyuso zao, vichwa vyao na vifua vyao na maji hayo ya kumwagika. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaambia: *"Kwanini mukafanya mambo hayo?".* Wakajibu: "kwa ajili ya kukupenda wewe, pengine Allaah nae atatupenda nasi Ewe Mjumbe wa Allaah.". Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema*: "Mukipenda kwamba Allaah na Mtume wake wawapende nyinyi, basi endeleeni kuwa na sifa sampuli tatu: Maneno ya ukweli, kutekeleza amana na kuwatendea majirani zenu wema. Lau jirani yako atadhuriwa, 'amali zako nzuri hufutika kama ambavyo Jua linavyoyayusha donge la barafu."* [No. 2998].

(Endelea Uk. 3)

(Endelea Kutoka Uk. 2)

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Kwa hakika kila Dini ina sifa na sifa ya Uislamu ni kuwa na tabia njema."* [No. 940].

Imepokewa na Abu 'Unbaah al-Khulaani katika riwaya itokayo kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Kwa hakika Allaah ana vyombo kutoka kwa watu wa hapa ulimwenguni. Vyombo vya Mola wenu ni nyoyo za watu wema. Vyenye kupendwa zaidi na Yeye miongoni mwavyo ni vile vilivyo Laini na vyenye Upole.* [No.1691].

Imepokewa kutoka kwa Jaabir nae amepokea kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa alisema: *"Kwa hakika, wenye kupendekeza zaidi kwangu miongoni mwenu na watakaokaa karibu yangu siku ya Qiyama, ni wale walio na tabia njema. Kwa hakika ninayemchukia miongoni mwenu na atakaekaa mbali na mimi siku ya Qiyama ni wale wenye kuzungumza maneno mengi ya urongo yasiyowahusu, ni wenye kuongeza yasiyokuwemo, na al-Mutafayhaqoon." Wakasema: "Sisi twajua yakwamba wenye kuzungumza maneno mengi ya urongo kuhusu mambo yasiyowahusu, ni wenye kuongeza yasiyokuwemo, lakini hawa al-Mutafayhaqoon ni kina nani?"* Akawajibu: *"Ni wale walio na kiburi."* [No. 791].

Fatima amesema: "Tulikwenda kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwatembelea wake zake. Kulikuwa na kiriba cha maji kikinin'ginia juu yake na maji yakawa yanatona juu yake, (katika riwaya nyengine: juu ya moyo wake), kutokana na homa kali iliyomshika. Tukamwambia: "Ewe Mjumbe wa Allaah! Si ungelimuomba Allaah, akakuponya?" Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: *"Kwa hakika watu wenye kupata mitihani mno ni Mitume, kisha ni wale wenye kuwafuata wao, na kisha ni wale wenye kuwafuata hao."* [No. 3267].

Amepokea Abdullaah aliyesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametuambia sisi: *"Kwa hakika, mutakuja kuwaona watu baada ya kuondoka mimi, watakuwa na tamaa ya sehemu ya Duniya na mambo yenye kuwachukiza nyinyi."* Wakajibu: "Sasa watuhimiza kufanyeje, Ewe Mjumbe wa Allaah?" Akajibu: *"Wapeni haki zao, nanyi mumuombe Allaah haki zenu."* [No.3555]

Amepokea Tawoos, aliyesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitaja alipokuwa juu ya minbar: *"Hapana shaka yakwamba Allaah ndiye mwenye kuongoza kwenye tabia njema na Yeye ndiye mwenye kumpotoa mtu mbali na tabia mbovu."* [No. 3255].

Imepokewa na Hani, aliyeuliza pindi alipokuja na kundi la watu kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Yaa Rasoolullaah, ni jambo gani litakalonilazimu mimi ili niingie Peponi?" Akamjibu: *"Unatakiwa uwe na maneno mazuri na utoe swadaka ya chakula."* [No.1939]

Amepokea 'Aaisha yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwambia: *"Kwa hakika, yoyote aliyetunukiwa sehemu ya Upole, atakuwa amepewa sehemu yake ya uzuri katika ulimwengu na Akhera. Kuwa na uhusiano mzuri na jamaa zako, tabia nzuri na kuwa mzuri kwa jirani zako hubariki makaazi yako na hurefusha maisha yako."* [No.519]

Amepokea Abdaah bin Hazn, aliyesema yakwamba wenye Ngamia walikuwa wakijigamba kuhusu utukufu wao kuliko wenye Kondoo. Kwahiyo, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: *"Musa (عليه السلام) alitumilizwa na alikuwa ni mchungaji. Daawud (عليه السلام) alitumilizwa na alikuwa ni mchungaji. Mimi nimetyumilizwa na ni mchungaji wa jamaa zangu karibu na mlima wa Ajyaad."* [No.3167]

Amepokea 'Amru bin Habeeb yakuwa alimwambia Sa'eed bin Khalid bin 'Amru bin 'Uthman: "Wewe ulikuwa wajua yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Mtumwa aliyevunjikiwa na kuharibikiwa, ni mtumwa ambaye Allaah amemkosesha rehma juu ya wana-adamu kwenye moyo wake."* [No.456]

Kila Sifa njema ni zenye kumstahiki Allaah, twamuomba amfikilizie swala Zake na salamu Zake Mtume wetu wa mwisho, Muhammad (صلى الله عليه وسلم), jamaa zake, Maswahaba zake na kila anayefuata uongofu wake hadi siku ya mwisho.

KUSWALI NYUMBANI KUTOKANA NA FITNA ZA NJE

Na: Sheikh Mash-hoor Hasan Aal Salmaan (حفظه الله)

NDUGU YETU KUTOKA DUBAI AULIZA:

Mimi ni kujana ninaeishi katika mji wa Dubai, naishi katika nyumba ambayo inakuchukua takriban dakika kumi kutembea mpaka msikitini. Hatahivyo, kama ujuavyo hapa mjini kuna fitna nyingi sana, kiasi cha kwamba inakuwa ni vigumu kwangu kutoka nyumbani isipokuwa huwa tunapambana na wanawake waliovaa mavazi yao vibaya na wakiwa wamejipamba. Sasa jee, naruhusiwa mimi kuswali nyumbani, nikiwa nafahamu yakwamba husikiya muadhini mara nyengine na mara nyengine huwa siusikii kutokana na makelele kwenye barabarani? Sasa iwapo nitaswali nyumbani, swala yangu hiyo itakubaliwa na swala zangu zilizotangulia zitakubaliwa?

JAWABU KUTOKA KWA SHEIKH MASH-HOOR (حفظه الله):

Laa Ilaaha Illa-Llaah! Sasa wewe waniuliza mimi kuhusu ruhusa ya kuswali nyumbani?! Hadeeth isemayo: *"Yoyote atakaesikiya muadhini na asiuitikie - basi hatokuwa na swala isipokuwa awe na sababu inayokubalika."* Basi wanavyuoni wanasema katika ufahamu wao wa hadeeth hiyo yakwamba iwapo muadhini ataadhini katika wakati wa kuanza kwa swala na akawa muadhini huyo ana sauti kubwa, na akaadhini kutoka kwenye jengo refu lisilokuwa na jengo jengine karibu yake (litakaloathiri sauti ya muadhini unaosikika) - basi yoyote atakaeusikiya wakati huo, na watu wote watakaousikiya, itawalazimu kuhudhuria swala ya jamaa'ah. Yoyote ambaye hatousikiya kutokana na umbali wao na mu'adh-dhin na wala isiwe ni kutokana na rabsha na makelele katika mazingara yake, basi huyu ndiye mtu asiyelazimika kuswali jamaa'ah (yaani atakuwa na sababu ifaayo). Hapana shaka yakwamba majengo marefu huathiri sauti lakini mfano sio namna hiyo, kwani iwapo kutakuwa na mtu ambaye mlango wa nyumba yake umeelekeana na msikiti na kando ya nyumba yake kuna wale wenye kuchimba mitaro, kwahiyo wakasababisha kelele nyingi, hapo pana uwezekano yakwamba huwenda asiusikie hata muadhini. Hatahivyo, hairuhusiwi kusema yakwamba hawajibiki kuswali swala ya jamaa'ah. Mafunzo kutoka katika, *"Yoyote atakaesikiya muadhini na asiuitikie."* inahusu mwanzoni unapoadhiniwa. Kwahiyo, ndugu yangu umesema, Baarakallaahu fiyk, yakwamba,

(Endelea katika Uk. 4)

"msikiti hauko mbali nawe, ni dakika kumi tu" na kwahivyo iwapo muadhini ataadhini kulingana na njia ya kimsingi iliyotajwa, utausikiya, basi swala ya jamaa'ah inakulazimu wewe.
Amma kuhusu fitna unazoziona, basi wewe usitoke nje ya nyumba yako kufanya yanayokupasa kuyafanya kuhusiana na chakula chako, kinywaji chako na shughuli zako? na ufanyapo hayo kwani wewe hujikurubishi na fitna? Sasa basi mbona wewe wazitaja fitna pale unapofika wakati wa kwenda kuswali tu? Ikiwa una uwezo wa kuithibitisha Dini yako na kuhofia fitna kwenye nafsi yako, basi ondoka hapo na hata kama ni kutoka mahali pamoja hadi pengine, au kutoka kwenye nyumba moja hadi nyengine. Hakuna kitu cha thamani alichomiliki mtu zaidi ya dini yake, na lau kitakuwa na usalama basi atakuwa amejikusanyia kombe la nguzo. Haifai kwa mja (wa Allaah) ajitie kwenye mitego ya fitna na kutokamana na Rehma za Allaah na waja (wa Allaah), kutokana na udhaifu wao, ni kwamba Allaah aliwaumba wao wakiwa wanamuhitaji Yeye na wabakie kuwasili baina ya mikono Yake na kwahiyo, akazifanya swala ili ziwape nguvu wasije wakatumbukia kwenye fitna. Kwahivyo, uwendapo msikitini, huwenda ukasikiya maneno mazuri na ukaja ukajuana na ndugu yako Muislamu aliye mwema, kwahiyo kuacha kwenda msikitini, hiyo ndiyo fitna! Kuepuka kwenda msikitini ndiyo fitna yenyewe!
Iwapo mja wa Allaah atasafiri, anajumuisha swala mbili pamoja, na kama hasafiri basi hajumuishi swala, na kama atakuwa ameukurubia msikiti basi itampasa aswali ndani ya msikiti ili asije Sheitwani akampatiliza kwenye ubora alo nao. Mja daima ni mwenye kumuhitaji Allaah ili usije uzuri wake ukakatika kutoka katika moyo wake, ili isije Rehma ya Allaah ikamkimbia mja huyu, swala ya faradhi imewajibishwa juu yake. Swala za faradhi daima na kudumu katika kubaki nazo ndio mambo yote ambayo yatakayomuepusha mja na fitna. Sasa hayo unayoyafikiria yatazidi kukuweka wewe mbali na Sheitwani atapata faragha na wewe, na hapo ndipo utakapokuwa ni kinyan'ganyiro chake. Miongoni mwa yenye kujenga nguvu za mja (wa Allaah), na Imani yake ni Jamaa'ah. Kwahiyo huruhusiwi, Akhee Abu 'Uthmaan, Baarakallaahu Fiyk, kuacha swala ya Jamaa'ah, haliyakuwa uko karibu na msikiti na Allaah Ndiye Mjuzi Zaidi.

NJIA NZURI YA KUWAITA WASOSWALI NA KUPAMBANA NA WAZUSHI

Shaykh Muhammad Salih Al-Munajjid

Ni ipi njia nzuri ya kuwaita wasioswali? Na vipi kuhusu wazushi?

JAWABU: Al-hamdulillah – **KWANZA:**

Twafaa tumzingatie yule anaeitwa kuswali au kufanya matendo mengine ya ibada, na kuwa mwangalifu kwa Njia yenye athari zaidi ya kumuhimiza au kumuonya. Misingi ya ki-ujumla katika Uislamu ni kujumlisha mambo yote mawili katika kuandamia (kuhimiza na kuonya) na ni muhimu vilevile kuzingatia alivyo laini mtu katika kuitikia mwito au kama ni mgumu ambaye aweza kuchukizwa na kuhubiriwa.

PILI: Njia bora ya kuwaita wale wasioswali yaweza kukusanywa kwa yanayofuatia: kuwakumbusha wajibu wa swala na kuwa ni nguzo iliyo tukufu kabisa baada ya Shahada mbili (*shahadatayn*).

Kuwaambia kuhusu uzuri wa swala, ni jukumu bora ambalo Allaah (سبحانه وتعالى) amewaamrisha waja Wake, na njia bora imfanyayo mtu kuwa karibu na Allaah (سبحانه وتعالى), Mola wake. Ni ya kwanza katika mas'ulia yake ambayo mtu ataletwa kuhisabiwa 'amali zake. Swala tano za kila siku ni zenye kufuta dhambi zenye kuja baina zao (swala), maadamu ajiepusha na madhambi makubwa. Sijdah moja yampandisha mtu kwa digrii moja na kufuta dhambi moja...na kuna mazuri mengine mengi yaliyotajwa katika hadeeth. Hili huenda likafungua kifua chake na pengine swala huenda ikawa ndio asli ya furaha yake, kama ilivyokuwa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kuwapa habari ya onyo kali lililotolewa kuhusu wasioswali, na maoni mbali mbali ya wanazuoni ikiwa hili ni miongoni mwa ukafiri na kuritadi. Uislamu haumpi mtu asiyeswali fursa ya kuishi huria miongoni mwa watu, kwa sababu kulingana na hali yake ni lazima aitwe kuswali, na aendelea kuwa *"taariq us swalah"*, atakiwa auawe kama murtadi kulingana na Kauli ya Ahmad (رحمه الله) na wengi ya waliokubaliana naye miongoni mwa Salaf, au auawe kama adhabu ya hadd, kulingana na Malik (رحمه الله) na ash-Shaaf'i (رحمه الله) au ashikwe na kufungwa, kulingana na kauli ya Abu Haneefah (رحمه الله) .Lakini hakuna mwanachuoni hata mmoja anayesema aachwe huru. Kwahivyo isemwe kwa yule asiyeswali: "Wewe unaraha yakuwa wanavyuoni wamekhitalifiana ikiwa wewe ni kaafir na ikiwa wafaa kuuawa au kufungwa? Kuwakumbusha kukukutana na Allaah (سبحانه وتعالى), kifo na kaburi na yatakayomfika yule asiyeswali, kwa jina mwisho mbaya na adhabu ya kaburi. Kujulishwa yakuwa kucheleweshe swala mpaka wakati ukapita ni katika madhambi makubwa: **[Lakini wakaja baada yao walio wabaya wakaacha swala, na wakafuata matamanio. Basi watakuja kuta malipo ya ubaya." [**MARYAM 19:59]. Ibn Mas'ud alisema kuhusu *"al-Ghayy"* (Jahanam): ni bonde lilioko Jahanam lililo na kina mno na kuna kionjo kibaya. Na Allaah (سبحانه وتعالى) Amesema: **[Basi ole wao wanaoswali *Ambao wanapuuza swala zao *Ambao wanajionesha *Nao huku wanazuia msaada." [**AL-MA'OON 107:4-5]. Kufafanua uzito wa kukata kauli yakuwa wao ni makafiri, kama kuhesabiwa ndoa zao kuwa ni Baatil, kukatazwa wao kubakia na wake zao na kustarehe nao. Na hakika yakuwa yeye hatooshwa atakapokufa wala kuswaliwa. Miongoni mwa maandishi yanayodhihirisha ni hadeeth ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: *"Baina ya mtu na Shirk na Kufr kwasimama kuacha kwake swala."* [Muslim #82]. Na alisema: *"Maagano tuliyonayo baina yetu sisi na wao ni swala; atakayeiwacha ni kaafir."* [Tirmidhi #2621 ;An-Nasaa'i #463; Ibn Maajah, #1079]. Kuwapa vijitabu na kanda zenye kuzungumzia madda ya swala na adhabu ya yule atakayeacha swala au simuangalifu katika swala zake.

Kuwakata na kuwaepuka ikiwa wataendelea na kutoswali. Ama kuhusu wazushi, namna tunavyo kabiliana nao yategemea sampuli ya Bid'ah inayohusika. Twafaa kuwanasihi na kuwaita kwa Allaah (سبحانه وتعالى), kusimamisha huja juu yao, na kuwarudi kwa kuwakanusha mijadala yao isiyo na mashiko. Ikiwa *mubtadee* atakazana na uzushi wake afaa akatwe na asusiwe, ikiwa yadhaniwa kuwa hili litamnufaisha yeye. Ni lazima tuhakikishe kuwa kwanza mtu ni *mubtadee* kabla hatujachukua hatua hizo, na maregeo yafanywe kwa wanachuoni kwa kuuliza kuhusu hayo. Nilazima tutafautishe baina ya Bid'a na yule anayeitenda, kwa sababu aweza kuwa na udhuru wa ujinga na kutoelewa. Kwa maelezo zaidi tafadhali tizama *"Haqeeqat al-Bid'ah Wa Ahkaamuhu"* muandishi ni Sa'eed ibn Nassir al-Ghaamidi.

Na Allaah ajuwa zaidi.